



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
ROBO YA KWANZA (JANUARI - MACHI) 2022,
BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha na Mipango
Julai 2022**

Yaliyomo

Majedwali	4
Orodha ya Vielelezo	5
Viambatisho.....	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Uchumi wa Dunia.....	1
1.2 Uchumi wa Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.....	1
1.3 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika	1
1.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki	2
1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania	3
1.5.1 <i>Pato la Taifa, Robo ya kwanza Mwaka 2022</i>	4
1.5.2 <i>Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya kwanza, Mwaka 2022</i>	4
1.5.3 <i>Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Kwanza Mwaka 2022</i>	5
1.5.4 <i>Mchango katika Kiwango cha Ukuaji, Robo ya Kwanza Mwaka 2022</i>	6
2.0 Ukuaji wa Uchumi kwa Shughuli za Kiuchumi.....	6
2.1 Kilimo, Misitu na Uvubi	6
2.1.1 <i>Mazao</i>	7
2.1.2 <i>Mifugo</i>	8
2.1.3 <i>Misitu</i>	8
2.1.4 <i>Uvubi</i>	8
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe.....	8
2.3 Uzalishaji Viwandani	9
2.4 Umeme	10
2.5 Maji	10
2.6 Ujenzi	11
2.7 Biashara na Matengenezo.....	12
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo	12
2.9 Malazi na Huduma za Chakula	13
2.10 Habari na Mawasiliano.....	13
2.11 Fedha na Bima.....	13
2.12 Upangishaji Majengo	14
2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundu na Sayansi	15
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala.....	15
2.15 Utawala na Ulinzi	15
2.16 Elimu	16
2.17 Afya	16
2.18 Huduma Nyingine za Jamii	16
3.0 Hitimisho	17

Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 20229

Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Kwanza Mwaka 2020 – 202213

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Kwanza 2021 na 2022	2
Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Kwanza Mwaka 2018 - 2022.....	3
Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2014 – 2022	4
Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Inayohusika	5
Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Kwanza Mwaka 2022	6
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Kwanza Mwaka 2021 na 2022.....	7
Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni), Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2022	11
Kielelezo Na. 8: Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Kwanza Mwaka 2017 – 2022	14

Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni	18
Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – Asilimia	20
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni	22
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) – Asilimia	24

1.0 Utangulizi

Taarifa za Pato la Taifa zinazotayarishwa kwa vipindi vyta robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina na kinachoaminika cha mwenendo wa uchumi kwa ajili ya kutathmini mabadiliko yanayotokea katika vipindi vifupi vifupi kwa ajili ya kutayarisha sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika Nchi.

1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya mwezi Aprili 2022, inaonesha kuwa uchumi wa dunia ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 3.6 kiwango ambacho kipo chini ya kiwango cha ukuaji wa asilimia 4.4 kilichokadiriwa kwenye ripoti ya mwezi Januari 2022 ambapo ni pungufu kwa pointi za asilimia 0.8. Makadirio ya ukuaji wa kiwango cha chini yanatokana na ukuaji hafifu wa uchumi kutokana na madhara ya vita inayoendelea kati ya Ukraine na Russia na pia madhara yanayoendelea duniani kutokana na uwepo wa UVIKO-19.

1.2 Uchumi wa Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara


Makadirio ya ukuaji wa uchumi miongoni mwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara yamekadiriwa kuwa asilimia 3.8 mwaka 2022 kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia ya Shirika la Fedha Duniani ya mwezi Aprili 2022. Ukuaji huu ni ongezeko la asilimia za pointi 0.1 ukilinganishwa na ukuaji uliokuwa umekadiriwa kwenye ripoti ya mwezi Januari 2022. Kwa sasa uchumi wa Nchi ya Afrika Kusini unakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 1.9 katika mwaka 2022 sawa na ilivyokuwa imekadiriwa kwenye ripoti ya mwezi Januari mwaka 2022. Vilevile, uchumi wa Nchi ya Nigeria umekadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 3.4 kwa mujibu wa ripoti ya mwezi Aprili 2022 ikilinganishwa na makadirio ya mwezi Januari 2022 ya ukuaji wa asilimia 2.7.

1.3 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika mwaka 2022, kwa mujibu wa ripoti ya mwezi Aprili 2022 inayotolewa na shirika la Fedha Duniani unatarajiwani kuimarika hadi kufikia asilimia 3.8 ambayo ni sawa na ongezeko la pointi za asilimia 0.1 ukilinganishwa na makadirio ya mwezi Januari 2022. Ukuaji

wa uchumi kwa baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kama vile Afrika kusini umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.0 kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2022 ukilinganishwa na ukuaji wa kiwango hasi cha asilimia 2.4 kipindi kama hicho mwaka 2021.Uchumi wa Namibia uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.3 katika robo ya kwanza mwaka 2022 ukilinganishwa na ukuaji wa kiwango hasi cha asilimia 4.9 kipindi kama hicho mwaka 2021. Uchumi wa Botswana ulikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 katika robo ya kwanza mwaka 2022 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Wakati huo huo, uchumi wa Tanzania umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.4 katika robo ya kwanza mwaka 2021 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Kwanza 2021 na 2022




Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2022

1.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimetoa taarifa za mwenendo wa uchumi katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 zimeonesha kuendelea kuimariika kwa ukuaji wa uchumi ambapo kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa Nchi ya Rwanda kimeongezeka hadi asilimia 7.9 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 3.5

katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Nchi ya Uganda imekuwa na ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.9 katika robo ya kwanza mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa kiwango cha asilimia 3.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Uchumi wa Nchi ya Kenya ulikua na kiwango cha asilimia 6.8 katika robo ya kwanza mwaka 2022 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, uchumi wa Tanzania umekua kwa kiwango cha asilimia 5.4 ukilinganishwa na asilimia 5.0 katika robo ya kwanza mwaka 2021. Nchi zilizobaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki bado hazijatoa mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika robo ya kwanza ya mwaka 2022.

Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Kwanza Mwaka 2018 - 2022



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2022

1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania


Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa robo ya kwanza (Januari - Machi) 2022 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za uchumi nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *2008 System of National Accounts*. Taarifa hii inahusu Pato la Taifa kwa Tanzania Bara kwa bei za mwaka husika na Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwanzoni mwa mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na za kila mwaka.

1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2022

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2022, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika liliongezeka hadi Shilingi trilioni 43.4 kutoka Shilingi trilioni 38.9 kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 liliongezeka hadi Shilingi trilioni 34.9 katika robo ya kwanza mwaka 2022 kutoka Shilingi trilioni 33.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 5.4.

Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2014 – 2022




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022

1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Kwanza, Mwaka 2022

Mchanganuo wa mchango katika Pato la Taifa kwa shughuli kuu za kiuchumi katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 unaonyesha kuwa, Shughuli za kiuchumi za Msingi

ziliwa na mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa wa asilimia 39.5, zikifuatiwa na shughuli za Huduma (asilimia 38.2) na shughuli za Kati (asilimia 22.3). Mchango wa shughuli kuu za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kabla ya kujumuisha kodi.

Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Inayohusika




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022

1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Kwanza Mwaka 2022

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022, Shughuli ya Usambazaji Maji safi na ukusanyaji wa majitaka ilikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ukuaji wa asilimia 11.9 ikifuatiwa na Fedha na Bima (asilimia 10.0), Huduma Nyingine za Jamii zinayo jumuuisha Sanaa na Burudani na Shughuli za Kaya katika Kuajiri ilikuwa na kiwango cha ukuaji wa (asilimia 8.5), Madini na mawe (asilimia 8.5), Umeme (asilimia 8.3), Habari na Mawasiliano (asilimia 8.0), na Utawala na Ulinzi (asilimia 6.1).

Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Kwanza Mwaka 2022



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022

1.5.4 *Mchango katika Kiwango cha Ukuaji, Robo ya Kwanza Mwaka 2022*

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022 zilichangia katika ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 5.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa asilimia 5.4 ziliikuwa ni pamoja na: Kilimo (asilimia 19.6), Ujenzi (asilimia 14.1), Viwanda (asilimia 9.0); Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 7.1); Biashara na Matengenezo (asilimia 6.7); na Fedha na Bima (asilimia 6.4).

2.0 Ukuaji wa Uchumi kwa Shughuli za Kiuchumi

2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvuvi


Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama. Shughuli hizi zinajumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.

2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 1.4 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji uliotokana na matumizi ya teknolojia na pembejeo bora; kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji na kuimarika kwa huduma za ugani.

Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Kwanza Mwaka 2021 na 2022



Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2022

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022, mazao yaliyokuwa na mchango mkubwa wa ukuaji yalikuwa ni pamoja na mpunga ambao uliongezeka kwa asilimia 18.9, kutoka tani elfu 465 mwaka 2021 hadi tani elfu 553 mwaka 2022; uzalishaji wa maharage ambayo yaliongezeka kwa asilimia 3.0 kutoka tani elfu 167 mwaka 2021 hadi tani elfu 172 mwaka 2022; uzalishaji wa mahindi uliongezeka kwa asilimia 2.6 kutoka tani milioni 2.7 mwaka 2021 hadi tani milioni 2.8 mwaka 2022; na viazi vitamu viliongezeka kwa asilimia 0.9 kutoka tani elfu 342 mwaka 2021 hadi tani elfu 345 mwaka 2022.

2.1.2 *Mifugo*

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022, uzalishaji wa mifugo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 kiwango sawa kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo ili kukidhi mahitaji ya bidhaa za mifugo kutokana na kuongezeka kwa wastani wa pato la mwananchi, ukuaji wa miji pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa lishe bora.

2.1.3 *Misitu*

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama vile asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikuwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 3.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.5 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na hatua za Serikali za kusimamia uvunaji endelevu wa mazao ya misitu.

2.1.4 *Uvuvi*

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia 1.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.8 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli ya uvuvi ulisababishwa na kuongezeka kwa kiwango kidogo kwa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

2.2 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa Madini na Mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini katika hali zake za yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (petroli) au

gesi (gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Pia inajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

- 1) Madini ya makaa ya mawe;
- 2) Petroli na gesi asilia;
- 3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- 4) Madini ya kokoto na mawe.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe kiliongezeka kwa asilimia 8.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 9.0 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya almasi, chumvi, fedha, makaa ya mawe na gesi asilia. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa almasi uliongezeka hadi karati 115,784 mwaka 2022 kutoka karati 3,571 kipindi kama hicho mwaka 2021 na makaa ya mawe yaliongezeka hadi tani 452,071 mwaka 2022 kutoka tani 190,932 katika kipindi hicho mwaka 2021.

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2022

Madini	Kipimo	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022
Gesi asilia	Mscf	11,980	12,710	13,729	16,138	14,573	14,432	18,401
Makaa ya Mawe	Tani	38,704	128,712	129,873	205,045	160,855	190,932	452,071
Madini ya Fedha	Tani	4,162	3,488	1,973	2,856	3,128	629	3,037
Chumvi	Tani	37,248	40,486	22,141	31,321	35,497	20,043	31,883
Almasi	Karati	77,959	69,897	97,497	117,187	104,749	3,571	115,784

Chanzo: Wizara ya Madini, 2022

2.3 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa

zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uzalishaji viwandani kiliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.3 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.1 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Pia inahusika na shughuli za usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozaishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali wa nishati ya umeme. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022, umeme uliosambazwa kwa wateja uliongezeka hadi saa za kilowati milioni 1,949 kutoka saa za kilowati milioni 1,800 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Shughuli ya uzalishaji umeme ilikua kwa kwa kiwango cha asilimia 8.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 7.2 kipindi kama hicho mwaka 2021.

2.5 Maji


Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi wa maji, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuweza kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozaishwa. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka

2022, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 86.9 kutoka mita za ujazo milioni 76.8 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji iliongezeka hadi asilimia 11.9 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022 kutoka asilimia 9.0 kipindi kama hicho mwaka 2021. Sababu zilizochangia ongezeko hilo ni pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya uzalishaji maji.

Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni), Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2022



Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, 2022

2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Shughuli ya Ujenzi inajumuisha, ujenzi wa nyumba za kuishi/makazi, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Ujenzi pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya

majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vyatia michezo.

Shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 5.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2021. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vyatia uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika shughuli za ujenzi. Kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo ambazo ni pamoja na chuma zilichangia ukuaji huo.

2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaaji wa jumla na rejareja (uuzaaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa za binafsi na za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Shughuli za Biashara na Matengenezo ziliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 kiwango sawa kama ilivyokuwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, bidhaa zilizozalishwa viwandani na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vyatia usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 9.0 kipindi kama hicho mwaka 2021.

2.9 Malazi na Huduma za Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya Malazi na Huduma za Chakula iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 6.5 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya malazi na huduma za chakula ilichangiwa na mahitaji ya huduma za utalii kutokana na idadi ya watalii waliongiza nchini kwa kipindi husika. Idadi ya watalii iliongezeka hadi 289,372 katika kipindi hicho mwaka 2022 ilikilinganishwa na watalii 231,131 kipindi kama hicho mwaka 2021.

2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji kwa mfano utangazaji wa radio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa taarifa.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Habari na Mawasiliano iliongezeka hadi asilimia 8.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.3 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa maongezi, huduma za ujumbe mfupi uliotumwa na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Kwanza Mwaka 2020 – 2022

Kiashiria, kwa Robo Mwaka	2020	2021	2022
Muda wa maongezi (dakika milioni) uliotumika	17,587	21,094	25,782
Ujumbe Mfupi (milioni) uliotumwa	32,424	32,795	34,612
Wateja wa fedha mitandao ya Simu, ('000') mwisho wa Machi	27,127	32,720	35,749


Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, 2022

2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma ya Fedha na Bima iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 10.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 2.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli ya Fedha na Bima ulichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 15.4 kwa amana kutoka shilingi trilioni 23.1 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 26.6 mwaka 2022; ongezeko la asilimia 15.0 la mikopo kutoka shilingi trilioni 20.0 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 22.9 mwaka 2022. Shughuli ya Bima peke yake iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 6.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 9.4 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Kielelezo Na. 8: Mikopo na Amana (Sh. Triliioni), Robo ya Kwanza Mwaka 2017 – 2022



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2022

2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoa na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Upangishaji Majengo kiliongezeka kwa asilimia 4.5 mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.6 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjinini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundu na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalam wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli za Kitaalam, Kisanyansi na Kiufundi iliongezeka kwa asilimia 5.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 7.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Kuongezeka kwa huduma za kisheria na uhasibu katika shughuli hii ya uchumi kulichangia kiwango cha ukuaji uliofikiwa.

2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni huduma za: kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa Huduma zinazohusiana na Utawala kiliongezeka kwa asilimia 6.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 7.4 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia zaidi ukuaji wa shughuli hii.

2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya Utawala na Ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Ukuaji wa shughuli ya Utawala na Ulinzi uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 6.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 kutoka asilima 2.4 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ya ukuaji ilitokana na ongezeko la matumizi ya fedha za Serikali

kulipia malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya Elimu iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli hii umetokana na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali katika utoaji wa elimu bila ada.

2.17 Afya

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha pia huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Shughuli ya utaoji wa huduma za afya iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji ilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma.

2.18 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya Sanaa na Burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya Huduma Nyingine za Jamii iliendelea kuongezeka hadi asilimai 8.5 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022 kutoka ukuaji wa asilimia 6.6 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko la watalii, idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii limechangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

3.0 Hitimisho

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2022, Pato halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 5.0 kipindi kama hicho mwaka 2021. Shughuli za uchumi zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji zilikuwa ni pamoja na: Usambazaji wa Maji Safi na ukusanyaji wa majitaka (asilimia 11.9); Fedha na Bima (asilimia 10.0); Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 8.5); Shughuli Nyingine za Kijamii zinayojumuisha Sanaa na Burudani na Shughuli za Kaya katika Kuajiri (asilimia 8.5); Umeme (asilimia 8.3) na Habari na Mawasiliano (asilimia 8.0).

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni

Mwaka	Nusu Mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biasara na Matengenezo	Malazi na Huduma ya Chakula	Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		28,008,976	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,821,248	1,525,619	7,815,845	1,824,471	4,115,393
2018		29,504,198	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,655,747	10,396,691	1,604,391	8,736,561	1,989,717	4,094,972
2019		30,802,027	5,485,112	10,184,558	994,879	510,411	17,802,021	10,965,038	1,645,950	9,493,191	2,133,312	4,281,167
2020		32,323,876	5,878,342	10,646,279	1,049,610	540,159	19,421,672	11,196,339	1,419,654	10,293,276	2,313,029	4,412,967
2021		33,577,189	6,442,881	11,155,762	1,154,204	575,213	20,256,410	11,590,493	1,514,711	10,658,344	2,524,564	4,629,490
2012	1	5,972,854	845,470	1,528,195	151,473	86,422	1,816,993	1,877,418	321,003	1,208,445	281,981	849,590
	2	5,182,996	825,383	1,544,666	164,427	89,319	1,808,760	1,855,404	320,427	1,456,176	303,507	844,631
	3	4,092,001	833,592	1,499,895	172,946	92,526	2,012,312	1,725,714	358,248	1,489,645	327,526	886,247
